

Je, uliwahi kujua . . .

Biblia iliandikwa na waandishi mbali mbali waliovuviwa na mbingu kwa kipindi cha miaka 1,500. La kushangaza ni kwamba, hii Biblia huelekeza kwa Yesu na kazi Yake kwa niaba yetu.

• *Hudumu Kama Yesu*

Jeshi la Wokovu ni shirika la kimataifa lililoko ulimwenguni kote lililojitoa kusaidia wenye mahitaji. Miaka kadhaa iliyopita walifanya congamano la kimataifa ambapo

mwanzilishi wa shirika hili, Generali William Booth, hakuweza kuhudhuria kwa sababu za kiafya. Hivyo akatuma ujumbe wake kwa kongamano hilo kwa njia simu ya upepo. Ujumbe ulikuwa wa neno moja: "WENGINE."

Kufanana na kuwa kama Yesu ina maana kuwajali wengine kwa lengo na dhamira tunayoionyesha. Kujitoa upya Kwake huhusisha kutenda. Wafuasi wake wanapaswa "kufungua vifungo vya uovu, kuzilegeza kamba za nira," na "kuwagawia wenye njaa chakula chako," na "kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako" (Isaya 58:6, 7). Watu wa pekee wa Mungu ndio mikono na miguu Yake ya kusaidia kukidhi mahitaji ya wengine.

Hatimaye, urafiki wako wa sasa na Yesu Kristo ndio kitu muhimu cha kutoa kwa wengine. Ni ukweli wa msingi kwamba kila muumini mpya atakuwa kiimani kadiri anavyoshiriki imani yake na wengine. Mwombe Mungu akuonyeshe mahitaji ambayo unapaswa kukidhi, ya kimwili na kiroho, na ndipo upige hatua ya kwanza kukidhi mahitaji hayo. Utashangaa jinsi ambavyo – Mungu atakuongoza kule anakotaka uende!

Basi, Mungu akubariki kadiri safari hii mpya ya kusisimua pamoja Naye inavyoendelea!



Share Him

Pata uzoefu wa jinsi nguvu za Mungu zilivyo kwa njia ya kushuhudia

Guide

Kwa ajili ya vitu vya kufanya siku ya sabato, angalia tovuti—www.guidemagazine.org

Karibu Katika Familia Ya Mungu!


Kwa hiyo umeamua kumfuata Yesu. Huo ni uamuzi ambao ungeweza kuufanya! Lakini sasa unafikiriaje? Hapa kuna mambo manne rahisi unayoweza kufanya ili kuendelea kukua katika imani ya Kikristo.

• *Weka Tegemeo lako katika Neema ya Mungu*

Ulipomwomba Yesu Kristo awe Mwokozi wako, neema Yake ilibakia kuwa sehemu ya maisha yako. Neema ni uwezo wa Mungu ufanyao kazi kwa niaba yako. Neema Yake hukuokoa, na karama hii hii itakusaidia kuishi maisha yatakayo kufanya uwe na furaha sasa na hata milele.

Neema ya Mungu yenye nguvu itakusaidia hata katika hali zo zote ngumu. Je, umekata tamaa? Je, unajaribiwa kutenda makosa? Je, unahitaji mwongozo kwa ajili ya wakati ujao? Muulize Mungu kwa njia ya maombi, na Yeye atafanya kwa niaba yako – kwa njia ya neema Yake.

Mungu anataka uelewe wazi kwamba siku zote neema Yake ipo kwa ajili yako. Ndio maana Biblia ina ahadi hii ya kusitajabisha:



Basi _____ na tukikaribie kiti cha

(Andika jina lako katika nafasi iliyowazi)

neema kwa ujasiri, ili _____ tupewe rehema,

(Andika jina lako Katika nafasi iliyowazi)

na kupata neema ya kusaidia _____ wakati

(Andika jina lako Katika nafasi iliyowazi)

wa mahitaji. (Angalia Waebrania 4:16).

Dai hii ahadi kila siku na unaweza kukabiliana na hali yo yote ile au nguvu za uovu za shetani.

• *Ibada ya Kila Juma*

Kisa kimeelezwa juu ya Francois Fenelon, muhubiri kwenye ikulu ya Mfalme Louis XIV wa Ufaransa katika karne ya kumi na saba. Mfalme pamoja na wasaidizi wake walikuwa wamewasili katika chumba cha ibada kwa huduma ya kila siku, lakini hakukuwa na mtu mwingine zaidi isipokuwa muhubiri pake yake. Mfalme Louis akauliza, "Hii ina maana gani?" Fenelon akajibu, "Mimi nilitangaza kwamba hutakuja kanisani leo, ili kwamba wewe Mheshimiwa uweze kujionea mwenyewe wale wanao mtumikia Mungu kihalali na wale wanao mhadaa mfalme."

Ni muhimu kuwapa na sababu sahihi za kuabudu: kumshukuru na kumheshimu Muumba na Mkombozi kwa kushughulikia maisha yetu na ulimwengu – sio tu kumfurahisha mtu fulani. Siku ya Mungu ya ibada, siku ya saba Sabato (angalia Mwanzo 2:2, 3; Kutoka 20:8-11), yapasa kuwa muda

Je, uliwahi kujua . . .

Pamoja na kisa cha bibliani, Yesu ametajwa na waandishi wengine kadhaa wa zamani. Mfano mmoja ni mwana historia wa Kirumi Cornelius Tacitus (55-120 A.D), ambaye aliandika, "Christus (Kristo) . . . aliteseka kwa adhabu kali kipindi cha utawala wa Tiberi katika mikono ya mmoja wa wazimamizi wake wa gereza, Pontius Pilatus" (Annals, 15.44).

mzuri wa kukusanyika kila juma kama familia ya Mungu. Husaidia kutufungamanisha pamoja katika "kusudi moja," na huwa ukumbusho uliyojaa furaha kwamba hatuhitaji kujaribu kujishughulikia wenyewe kwenda mbinguni: "Basi, imesalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake amestarehe

mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake." (Waebrania 4:9, 10). Kuiheshimu siku ya saba Sabato hakuleti pumziko la kimwili tu, lakini pumziko la kiroho pia.

Kwa sababu hiyo "tunatunzaje" Sabato katika nyakati za kizazi cha kisasa? Kutenga pembeni kazi, mahitaji na shughuli kwa kila siku ya juma ni mahali pazuri pa kuanzia. Kwa kufanya hivyo husaidia kuandaa mawazo yetu kutafakari upendo Mungu wa kustajabisha kwetu sisi. Kuabudu, kutumia muda kuangalia viumbe asili, kuomba, kusoma Biblia, kufurahia urafiki wa Kikristo na kuhudumia watu wenye mahitaji ni baadhi ya njia tunazoweza kutumia kumheshimu Mungu katika siku Yake ya pekee, Sabato.

• *Uwe Mwana Familia Anayewajibika*

Kama ilivyo familia ya duniani, kuwa mwana familia wa familia ya Mungu ni upendeleo na uwajibikaji pia.

Ni furaha iliyoje kujua kwamba tunaweza kutegemea hii familia yetu mpya kwa ajili ya upendo, msaada na kuhudumiana! Biblia huita "kujumuika pamoja," na kwa kawaida maana yake ni kushiriki pamoja na waumini wenzetu furaha na huzuni zetu.

Pamoja na kwamba Wakristo wanapaswa kuhudumia wanadamu wote, Biblia husema wazi kwamba lazima tutoe kipaumbele maalum kwa waumini wenzetu: "Kwa hivyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema; na hasa jamaa ya waaminio." (Wagalatia 6:10).

Je, katika uzoefu wako kama mwana familia wa duniani, matumaini yako yamepingua kwa namna ye yote ile? Familia ya kanisa yaweza kuleta uponyaji wa nguvu kadiri mnavyoshiriki kwa uwazi na kuonyeshana upendo usio na masharti ninyi kwa ninyi.

Ni muhimu kukumbuka kwamba familia ya kanisani inatokana na watu kama sisi wenyewe, wanadamu wanaokua na wasio wakamilifu. Nyakati fulani familia za aina zote hizo zaweza kutukatisha tamaa. Ndiyo maana lazima siku zote tuelekeze macho yetu kwa Yesu ambaye ndiye tu Mfano wetu halisi. Familia yako kanisani inakuhitaji. Fanya sehemu yako katika kushiriki upendo wako, muda wako, talanta zako, na vyanzo vyako vya kifedha pamoja na ndugu na dada zako katika Kristo.

